# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Namba za Simu-0623-735-416 Mkuu wa Shule-0767-703-143**

**Makamu Mkuu wa Shule-0626-408-510 Matron/Patron-**

**Shule ya Sekondari Chongolo**

**S.L.P.656**

**Bahi Dodoma**

**Tarehe ........................................**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI CHONGOLO HALMASHAURI YA BAHI MKOA WA DODOMA MWAKA ..........................**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ...................... na atasoma tahasusi ya ………….

**Shule ya Sekondari Chongolo** ipo katika kijiji cha **Chali Isanga** umbali wa Kilometa 74 kutokea makao makuu ya Halmashauri ya wilaya ya Bahi, na Kilometa 81 Kutokea Dodoma mjini. Usafiri wa basi kutoka Dodoma mjini unapatikana katika kituo cha mabasi **Kikuyu.**Nauli ni **Shilingi 7,000/=tu**.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ………….. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe .................... Mwisho wa kuripoti ni tarehe ..............................

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

**I.** Sare ya shule kwa Wasichana ni (Shati mbili(2) au zaidi rangi light blue mbili za tetroni za mikono mirefu lenye mfuko mmoja upande wa kulia).

**II.** Kizibao kimoja (1) rangi ya dark blue (material ni nyuzi za sweta) kwenye shingo ufito mweupe na chini ufito mweupe

**III.** Sketi mbili (2) Ndefu kitambaa cha suti aina ya draft (Mchanganyiko wa rangi ya maroon,nyeupe na nyeusi)Iwapo utaitaji maelezo zaidi piga simu namba 0767703143 na 0623735416.(Muhimu lizingatiwe kuepuka usumbufu).

**IV.** Sare ya Michezo ni raba nyeupe kwa ajili ya mazoezi na viatu rafiki kwa mchezo anaoupendelea mwanafunzi.

**V.** Tracksuit ya Kijani kwa PCB na PCM za blue zenye ufito mweupe pepembeni.

**VI.** Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

**VII.** Soksi jozi mbili nyeupe ndefu zaidi jozi mbili.

**VIII.** Wanafunzi wanao vaa hijabu (Kijumba) ziwe mbili (2) moja iwe nyupe na nyingine iwe blue bahari (Light blue) iwe ndefu kufikia usawa wa nyonga.

**IX.** Sweta rangi ya kijani kibichi(dark green).

**X.** Nguo za kushindia Sketi rangi ya kaki mbili(2) zenye malinda box.

**XI.** T-shirt 2 rangi ya kijivu nzito zenye kola(Form six) za kushindia zinapatikana shuleni kwa Tshs 15,000/=

**XII.** Sketi mbili za marinda ya kawaida ya kupanga kitambaa cha suti rangi ya ugoro

**XIII.** Tai ndefu rangi Nyeusi ya kufunga kila inapofuliwa.

**XIV.** T-shirt zenye nembo ya shule zinapatikana shuleni kwa shilingi elfu kumi na tano tu, mwanafunzi atapaswa kuja na kiasi hicho shuleni baada ya kulipia atakabidhiwa.

**XV.** Kwa mwanafunzi ambaye hajakatiwa bima ya afya anaweza kuja na shilingi 30,000/= ili akatiwe bima ya afya hapa shuleni.

***ZINGATIA***:Mwanafunzi hapaswi kuwa na Uniform nyingine zaidi ya zilizoainishwa hapo juu



**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari tisa (9) counter books (Quare 4), Kalamu, Mathematical **Error! Not a valid embedded object.**set, kalamu na calculator (fx-991).
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi nyeupe Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*Vitabu vya Taasisi ya Elimu Tanzania-TIE*).
iv. Godoro la ukubwa wa futi mbili na nusu.
v. Mashuka Jozi 2(Rangi ya pink), blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (*rangi njeupe cha pembe nne)*na mto wa kulalia.
vi. Nguo za ndani za kutosha
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
ix. Faili moja kwa ajili ya kuhifadhi kumbumbumbu za kitaaluma
x. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.

**ANGALIZO**: Mwanafunzi apangiwe kuleta kifaa kulingana na mazingira ya shule na tahasusi anayosoma.

**2.3 Michango mbalimbali kwa wanafunzi wa Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**2.4** Michango ilipwe kupitia akaunti ya shule ya bank ya **NMB** namba **52710016456** Jina la akaunti **Chongolo Sekondari**.Jina la mlipaji liwe jina la mwanafunzi husika na sio jina la mzazi/mlezi.Wakati wa kuripoti mwanafunzi awasilishe pay-in slip ya bank shuleni. NB: Mchango wa Uendeshaji wa Shule mwanafunzi atalipa kwa kila mwaka wa masomo.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya WAZIRI MKUU – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**
- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.**
- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu**
    1. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
    2. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
    3. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
    4. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA CHONGOLO SEKONDARI**

**Agapit C. Msowa**
**MKUU WA SHULE**

**NB:**
Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- **Mkuu wa shule 0623-735-416/0767-703-143**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0626-408-510**
- **Mwandamizi Malezi 0621155756**

FOMU NA 1 AHADI YA MZAZI/MLEZI

| |
|---|
| **BANDIKA PASPORT SIZE**<br><br>**YA**<br><br>**MZAZI/MLEZI** |

Mimi……………………………………………….mzazi/mlezi wa mwanafunzi…………………………………………ambaye ni Baba/Mama/Mlezi/ndugu (Ainisha uhusiano wako na mwanafunzi)……………………………..S.L.P…………………….

Mji…………………Simu……………….. na mwenye picha hapo juu. Ambaye kazi yangu ni....................................natamka hapa kama mzazi / mlezi wa ……………………... Ninakubali kwa hiari yangu mwanangu asome katika Shule ya Sekondari Kigwe kuanzia tarehe .............................................Ninaahidi kama ifuatavyo:-

1. Kwamba nimekubali chaguo alilopewa mwanangu na sitamruhusu kubadilisha hadi apate kibali cha maandishi kutoka kwa mamlaka husika.
2. Ninaahidi kumpatia mwanangu vifaa vyote kama vilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga ikiwemo SARE KAMILI ya shule bila kuharibu chochote.
3. Ninatambua ya kuwa walimu wanahitaji ushirikiano wangu katika kumpatia mwanangu elimu na nitashirikiana nao bega kwa bega kwa masuala yanayomuhusu mwanangu kitaaluma na nidhamu ili aweze kufikia malengo yake na ya Taifa.
4. Naahidi kuwa endapo mwanangu ataenda kinyume na taratibu zilizoainishwa katika fomu hii achukuliwe hatua stahili za kinidhamu kama alivyoorodheshewa.

Jina la mzazi/mlezi……………………………………………………………. saini……………………………….
Tarehe……………………………………

FOMU NAMBA 2 AHADI YA MWANAFUNZI

**BANDIKA PASPORT SIZE YA MWANAFUNZI**

Mimi…………………………………wanafunzi Wa kidato cha Tano tahasusi ……………… mwaka wa masomo ......................... Ninakiri kusoma, kuelewa na kuahidi kutii taratibu zote zilizoainishwa katika fomu iliyotumwa kwangu na Mkuu wa shule ya Sekondari Chongolo. Nitaheshimu sheria zote za shule na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa walimu na wasio walimu wangu na shule kwa ujumla katika muda wangu wote nitakaokuwa shuleni ili niweze kupata elimu na kuendeleza jamii na Taifa langu.

Jina:…………………………………………. Saini……………………………………..

Tarehe: ………………………………………….

FOMU NAMBA TATU (03) KIAPO CHA MZAZI/MLEZI

Mimi........................................................................................................ wa S.L.P…………………………Mji………………………..Simu Namba .............................................Nakiri kukaa na kuzungumza na mwanangu juu ya taratibu na sheria za shule na ninaahidi kumsaidia na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Mkuu wa Shule na walimu kwa muda wote ambao mwanangu atakapokuwa katika shule hii. Ninatambua madhara ya mwanangu kutembelewa na wageni wasioeleweka wakati akiwa shuleni na ninaomba shule iwatambue watu watatu (3) ambao wanahusika katika muda wote ambao atakuwa shuleni nao ni:- (ambatanisha picha passport size zao)

*PASPORTSIZE YA*

*NDUGU WA KWANZA*

JIna…………………………………………….kazi ya mzazi/mlezi/ndugu…………………………………Makazi……………………Simu…… ………………Uhusiano na mwanafunzi……………………………………………..

*PASPORTSIZE YA*

*NDUGU WA PILI*

Jina………………………………………….kazi ya mzazi/mlezi/ndugu………………………………Makazi……………………Simu....................................... Uhusiano na mwanafunzi……………………………………………………………..…..

*PASPORTSIZE YA*

*NDUGU WA TATU*

JIna…………………………………………….kazi ya mzazi/mlezi/ndugu…………………………………Makazi… ...........................Simu…… ………………Uhusiano na mwanafunzi…………………………….………..

**FOMU NAMBA NNE(4) UTHIBITISHO WA AFYA**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**CHONGOLO SECONDARY SCHOOL,**

**P.O. BOX 2993, DODOMA**

To be completed by Medical Officer from a known Public Hospital or Health Centre in respect to all entrants

Full name……………………...……………..Age……...Sex…………year…..

1. Blood count (Red and White) ……………………………………...
2. Urinalysis Test ……………………………………………………….
3. Syphilis test…………………………………………………………
4. T.B.…………………………………………………………………
5. Eye Test ……………………………………………………………
6. Ears…………………………………………………………………
7. Spleen………………………………………………………………
8. Abdomen ………………………………………………………….

ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical impairment, family disease, chronic infections etc.

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

I certify that the above named individual is fit to pursue studies as stated above

……………………………….. ……………………………………. Name and Designation Signature and Official stamp

……………………………….. ……….…………………… STATION DATE

## NOTE:

1. *Medical officer during the course of this Examination please attend the individual according to any diagnosed case.*
2. *The dully filled form must be handed to the Head of the School during registration week, under No circumstances should a student be registered without certification of his/her physical fitness.*